

KUENDA NJE YA KAMBI



Na tuendelea kusimama kwa muda mdogo tu.

Mungu mpendwa, tunakushukuru Wewe kwa majaliwa haya mengine ya kusimama katika nyumba ya Mungu na kumwabudu Mungu aliye hai. Tunashukuru sana kwamba tungali tuna ruhusa hii nchini. Na sasa tunashukuru kwa ajili ya watu hawa waaminifu, pia, Bwana, ambao wamekuja maili nyingi, mamia ya maili, wengi wao. Na baadhi yao watajaribu ku—kurudi nyumbani mbio, usiku wa leo, kwenye barabara kuu, kuvuka barabara kuu. Ee Mungu, naomba kwamba utakuwa pamoja nao na kuwasaidia. Waongoze, Ee Baba. Tunakushukuru kwa ajili ya manyunu haya ya mvua ambayo yametupoeza hewa, kwa muda tu.

² Pia, Baba, tunaomba kwamba utakutana nasi usiku wa leo katika Neno Lako. Kwa kuwa, hiyo ndiyo sababu tumekutanika, Bwana, ni kukutana Nawe katika Neno. Tusaidie, Bwana, ili kwamba kukutana kwetu kutakuwa na faida sana kwa Ufalme Wako, na ili kwamba tusaidike kiasi kwamba, tupate kuwasaidia na wengine. Yajalie mambo haya tunayoomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

³ Nimekuwa na mazungumzo ya faragha na watu wachache mle ndani. Na kabla tu ya mkutano kuanza, Billy alinipa lundo—lundo kubwa sana lake hata ni vigumu kwa—kwangu kujua nitaanzia wapi. Bali tunaomba kwa—kwamba Mungu atawabariki kwa juhudi zenu za kungojea ibada ya jioni.

⁴ Sasa, Mungu akipenda, Jumapili ijayo asubuhi nitakuwa na i—ibada tena. Ndiyo kwanza nizungumze na mchungaji, na ni vema kwao.

⁵ Na sasa natamani ningaliweza kumtambua kila rafiki mwema niliye naye humu ndani, ila ninajua ya kwamba mnangojea. Kuna joto. Na ni—nitaacha tu wakati huo, na—na kusema tu hivi, “Mungu awabariki.”

⁶ Mnajua, sijui jambo lo lote kubwa zaidi ambalo mtu ye yote angeniombea, kuliko kusema, “Mungu akubariki.” Mnaona? Kama atafanya hivyo, hilo tu ndilo ninalohitaji, hilo—hilo tu. Nafikiri hilo ndilo neno kuu sana ka—katika msamiati, “Mungu akubariki.” Na, sasa, nami najua Yeye hufanya hivyo.

⁷ Na kama nilivyomwambia mke wangu muda mchache uliopita. Nilikuwa—nilikuwa nikijaribu kuoga, nami singeweza kukauka. Ninge—ningekauka, halafu nikalowa tena. Ningekauka, na singeweza kuvaa shati langu, hata. Na ni tofauti kidogo huko Tucson. Kuna joto karibu mara mbili ya hapa, bali

hu—hutokwi na jasho yo yote. Hamna u—unyevu hewani, kwa hiyo inaikausha mara tu unapotoka nje. Unaweka sufuria ya maji kule, na mara yamekauka. Huwezi kutokwa na jasho, sababu inakaushwa kabla hu—hujatokwa na jasho. Unatokwa na jasho, kweli, bali hulioni kamwe. Kwa hiyo, hapa, nilikuwa nikijaribu kuwa na wakati mbaya sana nikikauka. Kwa hiyo, na ni—ninalowa sasa hivi.

⁸ Nilikuwa nimerudi chumbani mle, nasi tulikuwa na watu saba au wanane mle ndani, ambao walikuwa dharura, na ambao ilibidi waonwe mara moja.

⁹ Naam, sababu ya kunifanya nikae, na kuwaombeni m—mje, ni kwa kuwa na—najisikia ina—ina manufaa kwetu. Ni—nisingefanya jambo hilo, enyi marafiki. Na—nawathamini sana, kufanya hivyo, kuja tu ku—kumsikia mtu fulani, ama kusikia yale ninayosema, ama lo lote lile. Ni—nisingefanya hivyo. Hilo halingekuwa halali. Halingeonyesha upendo wangu kwenu, kuja tu namna hiyo. Nami siamini ya kwamba mnakuja... Ingawaje, najua mnanipenda, kama ninavyowapenda ninyi. Na—na kwa hiyo na—na—najua hivyo, la sivyo hamngefanya mambo mnayofanya. Kwa hiyo nawawazia vya kutosha, hata nisingewaacha mkae katika joto na kadhalika, namna hii, kama sikufikiri ni jambo fulani la kuwasaidieni.

¹⁰ Halafu, kabla ya kuja hapa, daima najaribu niwezavyo, mbele za Mungu, kuchukua kitu kidogo, Andiko la namna fulani, kisha naomba uongozi Wake, jambo la mwisho kabla ya kuondoka. “Nisidie, Bwana Mungu, kwa namna fulani, wa—wape hao watu wapendwa cho chote uwezacho.”

Nami natarajia, na ninaamini, ya kwamba daima nitaishi pamoja nanyi. Naamini ya kwamba huu ndio muda mdogo sana tulio nao, tunaposimama pamoja namna hii. Tutakuwa pamoja katika Umilele. Mnaona? Nafanya hivyo. Na—na—naamini hivyo.

Nami nataka kuwasaidia. Nami, kama nikisema jambo lo lote baya, Baba wa Mbinguni anajua si kwamba nataka kufanya hivyo; ni kwa sababu nafanya hivyo bila kujua; ningefanya hivyo kwa kutokujua.

¹¹ Kwa hiyo, nikijua ya kwamba ninyi mko chini ya daraka langu, na mko mikononi mwangu, kwa ajili ya Injili, daima nitataka kuwaweka katika kurasa za Biblia hii. Na—nami na—...

Mara nyingi watu wamenijia, na kusema, “Ndugu Branham, kama tu utakuja hapa na kusema ‘BWANA ASEMA HIVI’ kwa mtoto wangu aliye mgonjwa, atapona. Uondoke uende kule useme tu, ‘Atapata afya.’ Hivyo tu ndivyo ninavyokutaka ufanye.”

¹² Naam, huo ni uaminifu na ni jambo la kupendeza. Jinsi ninavyothamini jambo hilo! Lakini, mwajua, siwezi kufanya

hivyo mpaka atakaponiambia, kwanza. Mnaona? Naweza kumwombea huyo mtoto, nifanye yote niwezayo.

Lakini, mnaona, vipi kama nilienda kule na shauku na kusema hivyo? Mnaona, kama nilisema, “BWANA ASEMA HIVI,” kweli ingekuwa tu shauku yangu yasema hivi. Mnaona? Mnaona? Na halafu huenda ikatendeka, na huenda isitendeke. Lakini, basi, vipi kama mtu yuyo huyo yuko chini ya shauku yangu, na haikutendeka? Halafu, mtu huyo huenda akawa katika ha—hali wakati mwingine ya kati ya uzima na mauti, basi matumaini yao yatakuwa wapi? Wangehofu kwamba huenda nikawa katika shauku yangu tena. Mnaona?

Kwa hiyo, ninapotamka hayo, nataka kuwa na hakika kabisa kwamba ni kweli, kwa yote niyuayo. Kisha anaponizungumzia, naweza tu kusema yale aliyonionyesha. Yawe mazuri au mabaya, sina budi kuyasema. Na wakati mwingine si—si vizuri kuwaambia watu mambo hayo. Lakini, hata hivyo, ninawajibika tu kuwaambia watu ma—mambo mabaya yatakayowapata, kama ninavyowajibika kuwaambia mambo mema yatakayowapata.

¹³ Na, hata hivyo, tunataka mapenzi ya Bwana. Wakati mwingine mapenzi ya Bwana kinyume cha haja zetu. Bali, hata hivyo, kama tukitaka mapenzi ya Bwana, ni muhimu tu vile vile kujua kwamba mabaya yatatupata, kama yakiwa ni mapenzi ya Bwana. Kama ni mema ama mabaya, tunataka mapenzi ya Bwana yatendeke. Nami najua ya kwamba tunaliangalia kwa jinsi hiyo.

¹⁴ Sasa, na—najua ndugu hapa kwa kawaida huwa na ujumbe wa dakika thelathini, dakika ishirini hadi thelathini Jumapili usiku. Nami si—sijui kama naweza kufanya hivyo au la, kwa hiyo ni—nitafanya niwezavyo.

¹⁵ Sasa, nafikiri kuna ibada ya ubatizo mara baada ya haya. Nasikia walibatiza kundi kubwa la watu asubuhi ya leo. Daima, kuna ubatizo unaofanyika hapa, wakati wote. Wahudumu, Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, church of God, Waluteri, wo wote wale, wanakuja na kubatizwa katika Jina la “Bwana Yesu Kristo.”

Na mbele za Mungu, itakaponilazimu kusimama mbele ya ile Hukumu, nitawajibika kwa jambo hilo. Na kama nilikuwa na hakika niani mwangu, ya kuhesabiwa haki katika kila kitu maishani mwangu kama nilivyo kwa jambo hilo, ningekuwa tayari kwa ajili ya Kunyakuliwa sasa hivi, kwa kuwa najua hiyo ni Kweli ya Injili. Mnaona? Hiyo ni Kweli.

¹⁶ Hakuna Andiko hata moja katika Biblia ambapo mtu ye yote alibatizwa kwa njia nyingine yo yote ila katika Jina la Yesu Kristo. Lile agizo la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” ni tu. . . “Enendeni basi, makayafanye mataifa yote wanafunzi, mkiwabatiza katika *Jina* la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Sio

katika...si kukiitia cheo hiki juu yao; bali kuwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, ambalo ni “Bwana Yesu Kristo.”

¹⁷ Kila mtu katika Biblia alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, “Ye yote atakayeliiondoa Neno moja Kwake, au kuongeza Neno moja Kwake, kwa njia yo yote, ole wao.” Kwa hiyo ninayo ya kutosha kuhofu, mbali na kuongeza ama kutoa katika Maandiko.

Imenitia katika shida mara nyingi, bali mimi nadumu papo hapo. Yeye ndiye mtetezi wangu. Iisababisha kutengana na marafiki wengi. Wamejitenga nami kwa ajili ya jambo hilo. Bali mradi tu namweka Rafiki huyu hapa, Bwana Yesu! Naye ni Neno. Haidhuru, hata njia iwe yenye kuparuzia namna gani, hata njia iwe ngumu vipi, Yeye huja vile vile. “Na kama wakimwita Bwana mwenye nyumba ‘Beelzebuli,’ ni zaidi sana vipi watawaita hao wa wanafunzi Wake!”

¹⁸ Sasa Bwana awe nanyi nyote na awabariki juma nzima, na awape ninyi nyote mambo yaliyo mema sana ambayo naweza kuomba kwamba Mungu awape, ndiyo maombi yangu.

Sasa tutasoma kutoka katika Neno la thamani.

¹⁹ Na—na sasa kumbukeni, tena, Jumatano usiku... Kuna maombi ya katikati ya juma au cho chote kile? [Ndugu Neville anasema, “Jumanne, mkutano wa maombi ya nyumbani, Jumatatu na Juamane usiku.”—Mh.] Jumatatu na Jumanne usiku ni mikutano ya maombi ya nyumbani. Nadhani watu wanajua.

²⁰ Ndugu Junior Jackson, yuko kwenye jengo hili? Mimi... Ndugu Jackson, si-... [Ndugu Neville anasema, “Ndiyo, papa hapa.”—Mh.] Yuko hapa, Ndugu Jackson. Vema. Ni—ni-... Ndugu Jackson mwingine hapa, ni-...

Na Ndugu Don Ruddell, yuko kwenye jengo hili usiku wa leo? Ndugu Don, upande huu hapa.

Na wengi wa hao ndugu wengine, nawaona ndugu hapa kutoka Arkansas, na Louisiana, na—na mahali mbalimbali nchini.

²¹ Nami nina wengine, ndugu wazee hapa usiku wa leo, pia. Nina Ndugu Thomas Kidd anayeketi hapa mkono wa kulia, atakuwa na umri wa miaka themanini na minne katika siku chache. Na yapata miaka mitatu au minne iliyopita, alifanyiwa upasuaji kwa ajili ya ugonjwa wa kibofu, na alikuwa akifa kwa kansa. Madaktari walikuwa ndio kwanza wamrudishe akafe. Nami karibu niliharibu gari langu kuukuu, nikienda kwake, kule Ohio. Ndipo Bwana Yesu akamponya akawa mzima na mwenye afya. Huyu hapa, yeye ana maskini mwenzi wake, usiku wa leo. Na wengi wenu mnawajua; labda baadhi yenu hamumjui. Bali huyu hapa mwanamume na mwanamke aliyekuwa akihubiri

Injili kabla sijazaliwa. Wazia jambo hilo, nami ni mzee. Mnaona? Naam, nawaangalia, nao wangali wanaendelea, ndipo inanitia moyo.

Sisi sote tunamjua Ndugu Bill Dauch anayeketi hapa pembeni.

²² Na, loo, jinsi tunavyoshukuru kwa baraka zote kuu za Mungu! Na ziendeleo kuwa pamoja nasi hata hiyo parapanda ya mwisho itakapolia na, mwajua, “Tutanyakuliwa pamoja, kumlaki Bwana hewani,” Liwazieni! Watawakosa watu, hawawezi kuwaona tena, bali mnakusanyika pamoja na kundi lile lingine lote.

“Hao walio hai na waliosalia hata kuja kwa Bwana hawatawatangulia, ama kuwazuia,” ndilo neno, “hao waliokwisha kulala mauti,” si waliokufa. La, Wakristo hawafi. Wao wanapumzika kidogo tu, mnaona. Hivyo tu. Loo, jamani! “Na parapanda ya Mungu italia; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza,” wawatokee wengi. Na mara moja, inatokea kwamba unasimama na kuangalia, na, vema, huyo hapo ndugu fulani, nawe unajua haitachukua muda mrefu. Katika dakika chache, “Tutabadilika, katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho. Kisha sisi pamoja nao tutakosekana duniani, tutanyakuliwa kumlaki Bwana hewani.”

²³ Na, kuwazia, kwa yote ambayo tumeona katika Maandiko, na mathibitisho wazi ya saa hii tunayoishi, yaweza kutukia kabla ibada hii haijaisha, wazia hilo tu, usiku huu.

Basi, kwa hayo, tunalikaribia Neno Lake, huku tukifungua Waebrania sura ya 13, nasi tutasoma kuanzia aya ya 10 hadi ya 14. Ya Waebrania 10 na...au, au samahani. Waebrania 13:10 hadi 14.

²⁴ Sasa, kama nilivyosema, sisi, tunapoonyesha utii wetu kwa bendera yetu, jambo ambalo ni zuri, mimi...Daima tunasimama tunapoonyesha utii wetu. Na matukio mengine yote makuu, tu—tunasimama katika kuiheshimu, ama kuipigia saluti, na kadhalika, kwa taifa letu. Na wanapouimba *Bendera Iliyopambwa Nyota*, tunasimama sawasawa.

²⁵ Nasi kama askari Wakristo, hebu na tusimame sawasawa tunapolisoma Neno la Mungu. Sikizeni kwa makini tunapolisoma Neno. Sababu ya kutaka kulisoma; maneno yangu huenda yakashindwa, bali Yake hayatashindwa. Kwa hiyo kama nikisoma Neno Lake, peke yake, mtabarikiwa. Aya ya 10 ya sura ya 13 ya Waebrania.

Tuna madhabahu ambayo wale waihudumiao ile hema hawana ruhusa kula vitu vyake.

Maana wanyama wale ambao damu yao huletwa ndani ya pale patakatifu na kuhani mkuu kwa ajili ya dhambi, viwiliwili vyao huteketezwa nje ya kambi.

Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango.

Basi na tutoke twende nje ya kambi, tukichukua shutumu lake.

Maana hapa sisi hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao.

²⁶ Bwana Mungu, Wewe ambaye unawajibika kwa Neno hili, na unawajibika kulitunza kote katika nyakati zilizopita, kuona kwamba linatufikia bila kughoshiwa. Ni Neno la Mungu lililo safi na ambalo halikughoshiwa. Sisi tunalithamini sana mioyoni mwetu wakati huu. Livunje somo hili, Bwana, katika maana yake kwa ajili yetu usiku wa leo; kusudi sisi, wana wa wanadamu, tupate kufahamu matakwa ya Mungu. Maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

²⁷ Somo langu kwa ajili ya ji—jioni ya leo ni: *Kuenda Nje Ya Kambi*. Ni somo dogo kweli, kidogo ni la kipekee, lakini, mwajua, kwa kawaida tunampata Mungu katika mambo yasiyo ya kawaida. Ulimwengu unashikilia desturi sana, hata, jambo lo lote lisilo la kawaida kutoka kwa mwelekeo wa kawaida, linakuwa la kipekee.

Kama nilivyohubiri hapa siku chache zilizopita, hapa katika Maskani, juu ya: *Wa Kipekee*. Na mkulima ni wa kipekee kwa mfanyi biashara; mfanyi biashara ni wa kipekee kwa mkulima. Mkristo ni wa kipekee kwa -amini . . . asiyeamini, na kadhalika. Huna budi kuwa mpumbavu kwa mtu fulani. Kwa hiyo, cho chote kisicho cha kawaida, kinakufanya mpumbavu kwa namna fulani, kwa—kwa mwelekeo wa kawaida.

²⁸ Na kwa hiyo, watu wa Mungu, na manabii Wake, na wajumbe Wa—Wake kote katika nyakati, ambao waliubeba Ujumbe Wake kutoka kwenye Neno, wamehesabiwa kuwa wajinga, kwa watu wa nje.

²⁹ Nuhu alikuwa mpumbavu, kwa ulimwengu wake wenye akili nyingi ambao aliuhubiria. Nuhu . . . Alikuwa kweli mpumbavu, kwa Farao; huku mguu wake umo kwenye kiti cha enzi halafu anakiacha, akachagua kundi la wakanyanga matope, kama walivyofikiri. Pia Yesu alikuwa mpumbavu, kwa watu. Na hao wengine wote ambao wamefanya kazi na kumwishia Mungu, wamehesabiwa kama wapumbavu. Hawana budi kwenda nje ya kambi waliyokuwa nayo.

³⁰ Zaidi na zaidi, ninafanywa kuamini ya kwamba watu hawamfikii Kristo.

Sasa, niko hapa kujaribu kusaidia katika njia yo yote niwezayo, na kufanya matamshi yangu dhahiri nijuavyo jinsi ya kuyafanya. Nanyi mnivumilie mkiweza.

³¹ Ninapoangalia na kuhubiri nchini kote, na kuwaangalia watu, ni—nimeshawishika kabisa ya kwamba watu hawamfikii

Kristo. Nami naamini ya kwamba adui ndiye amewatupia kizuizi hiki. Kwa maana, sababu ya kuamini jambo hili, Yeye siye kitu walichoelekezwa kwake. Aidha wameelekezwa kwenye fu—fu—fundisho la sharti, ama fundisho fulani, ama karamu fulani, ama tukio, ama msisimko fulani, ama kitu kama hicho, badala ya kuelekezwa kwa Kristo, aliye Neno.

Hiyo ndiyo sababu nafikiri watu wanaweka kikomo chao cha Milele juu ya mafundisho fulani ya sharti, ama msisimko fulani. Kama vile, wengine husema, “Nilicheza katika Roho. Ama, “Ni—niilinena kwa lugha. Ni—ni—nilihisi moto ukipitia juu yangu.” Na je, wajua, vitu hivyo vyote vinaweza kuigizwa na ibilisi?

³² Kuna kitu kimoja tu asichoweza kuigiza, hicho ni Neno. Katika yale mabishano, kati yake na Yesu, kila wakati Yesu alimshinda. “Imeandikwa,” Neno!

Nami naamini, leo, ya kwamba sababu ya watu kutokuja kwa Kristo, ni kwa sababu wanaelekezwa, wengi wao, kwenye madhe—dhe—dhehebu. “Njoo ujiunge na kanisa letu.” Ama, “Wewe soma katekismo yetu,” ama, “Uamini fundisho letu,” ama—ama namna fulani ya taratibu. Wao wanaelekezwa upande mbaya. Na matendo yao na maisha wanayoishi bila ya Kristo, yanathibitisha maishani mwao, yanathibitishwa na jambo lile lile.

³³ Kwa mfano. Sitaki kumuudhi mtu awaye yote. Lakini, nenda rudi, kila mahali nchini, nimewakemea wanawake kwa kuwa na nywele fupi. Hiyo ni Biblia. Nimewakemea wanawake kuvalia kaptura, kutumia vipodozi. Na kila mwaka inazidi kuwa mbaya. Inaonyesha ya kwamba kuna kidole kingine, mahali fulani, kinachowaelekeza kwenye njia nyingine. Nao hawamfikii Kristo.

³⁴ Nao wanasema, “Sisi ni washiriki wa kanisa fulani. Kanisa letu hali- . . .” Haifai kitu kanisa lenu linaamini nini.

Mungu alisema, “Ni kosa.” Na kama walifika kwa Kristo, wangekomesha jambo hilo. Na, isitoshe, bali mtu angepachukua mahali pake kama angelimfikia Kristo, na akalipinga jambo hilo. Wanaume hawangewaruhusu wake zao kutenda jambo kama hilo. Mtu halisi hataki mke wake kufanya hivyo.

³⁵ Maskini jamaa mdogo hapa mjini, juzijuzi, nusura awaue wavulana wawili wadogo. Walikuwa kwenye kituo fulani cha petroli. Ninyi watu wa Jeffersonville mliliona katika gazeti. Naye huyu msichana mdogo alikimbia kwenye kituo cha petroli, hajavaa kitu, karibu uchi, kabisa, nao hao vijana wawili waliokuwa wameketi pale wakasema kitu. Na yule mtumishi karibu awauwe hao wavulana wawili; ndipo akashikwa kwa ajili ya jambo hilo, akapelekwa mahakamani. Basi hakimu akamuuliza, “Kwa nini uka- . . . yeye alivalia namna hii?”

Akasema, “Nafikiri anaonekana mrembo sana.”

³⁶ Sasa, huyo mtu ana kasoro. Sijali kama yeye ni . . . Kama yeye ni mwenye dhambi, ana kasoro. Upendo wake kwa mwanamke huyo haungeweza kuwa halisi, naye anamweka huko awe chambo cha mbwa namna hiyo. Kuna kasoro. Je, wanadamu wamefikia ufahamu kwamba wangeweza kupambanua kati ya mema na mabaya?

³⁷ Je, mmeona lile vazi jipya la kuogelea walilotoa? Mnajua ubashiri wangu kwamba wanawake hatimaye watafikia majani ya mtini, miaka thelathini na mitatu iliyopita? Na sasa wanao ambao wamevalia majani ya mtini tena, marinda yanayoona. Neno la Bwana halishindwi. Mnaona? Na hilo lilikuwa litukie kabla tu ya wakati wa mwisho, watarudia jani la mtini tena. Nilikuwa nikisoma jambo hilo katika gazeti la *Life*. Hilo lilisemwa miaka thelathini na mitatu iliyopita, kabla ya kuanguka kwa wanawake. Ilisemwa jinsi wangepanya jambo hilo katika siku hii, na sasa wanalitimiza. Jinsi wangepalia mavazi kama wanaume, na jinsi wata-. . . Uadilifu wa wanawake utashuka katika taifa hili.

³⁸ Taifa duni sana ulimwenguni, ni hili la Marekani. Ndilo chafu sana katika kundi hilo. Hiyo ni kulingana na takwimu. Visa vya ndoa na talaka katika taifa hili ni vingi sana kuliko mahali pengine po pote ulimwenguni, na mataifa mengine yanaliiga. Tulikuwa tukiiga Ufaransa, uchafu na vinyaa vya taifa hilo, na sasa wao wanatoa mavazi yao kutoka kwetu. Tulivuka mpaka wao.

³⁹ Ninajua kuna sababu ambazo watu hawamfikii Kristo. Kama wangelimfikia, hawangetenda hivyo.

Yesu aliteswa nje ya lango, ili kwamba awatakase watu kwa Damu Yake Mwenyewe. *Utakaso*, linatoka kwenye neno la Kiyunani, lenye maana mbili, ambalo linamaanisha, “kuoshwa, na kuwekwa kando kwa matumizi.” Na wakati Mungu anapowaosha watu Wake kwa Damu ya Yesu, Yeye huwaosha na uchafu wa ulimwengu na kuwaweka kando kwa ajili ya utumishi.

Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango.

⁴⁰ Hata watu wa Full Gospel, wamerudi moja kwa moja kwenye lile shimo tena walimotoka. Kanisa la Kipentekoste lilikuwa nini, miaka arobaini ama hamsini iliyopita? Waliyalaani, wakayahukumu, wakayacheka makanisa waliyotoka, hayo madhehebu. Walifanyaje? “Kama tu mbwa kwenye matapiko yake, na nguruwe katika kugaa-gaa kwake.” Walirudi moja kwa moja kwenye mahali pale walipotolewa, na sasa makanisa yao ni machafu tu kama yale mengine.

⁴¹ Ilikuwa kitu fulani, kama nilivyosema asubuhi ya leo. Kama vile, watu wako kama alivyosema Petro, katika Mathayo

Mtakatifu—Mtakatifu 17:4 hadi 8, ambapo alisema, “Ni vizuri sisi kuwapo hapa. Na tujenge vibanda vitatu.”

⁴² Lakini Roho akamkataza kufanya hivyo. Kasema, “Huyu ni Mwanangu, Mpendwa Wangu; msikieni Yeye,” naye ni Neno. Huyu Ndiye tunapaswa kumwagalia, Neno, si shauku yetu ama kitu kingine. “Yeye ni Neno Langu; msikieni Yeye!” Nao waliona nini baada ya Sauti hii kunena nao? Hata Musa na Eliya hawakuweco; wala hapakuwepo na kanuni ya imani; wala hapakuachwa kitu ila Yesu pekee, Naye ni Neno. Hilo tu ndilo waliloona.

Sasa, “Kutoka nje ya kambi.”

⁴³ Tunaona ya kwamba katika kambi yao mahali jambo hili kuu lilipotukia, kule juu katika Mlima wa Kugeuzwa, kama Petro alivyouta baadaye, “mlima mtakatifu,” mahali Yeye alipokutana nao. Naam, siamini ya kwamba huyo mtume alimaanisha ya kwamba huo mlima ulikuwa mtakatifu; alimaanisha ilikuwa ni Mungu mtakatifu kwenye huo mlima.

Si kanisa takatifu; si watu watakatifu. Ni Roho Mtakatifu katika watu. Roho Mtakatifu ni mtakatifu. Yeye ndiye msimamizi wako na kiongozi wako.

⁴⁴ Nasi tunaona, katika kambi hii ndogo kwenye mlima, wa Kugeuzwa, walipoagizwa kusikia, kitu tu walichoagizwa kufanya ni kusikia Neno. Kitu pekee walichokiona, si kanuni ya imani. Hawakuona kitu ila Yesu, Naye ni Neno lililofanyika mwili.

Jinsi hilo lililivyo zuri, kwa kambi ile ile iliyokuwa katika bustani ya Edeni. Mungu alipolifanyia ngome kanisa Lake katika bustani ya Edeni, watu Wake, walikuwa wakingwe na ukuta mmoja; huo ulikuwa Neno. Walikuwa na ngao moja, silaha moja, kitu kimoja, kwa maana Mungu alijua ni nini kingemshida ibilisi, nacho ni Neno.

⁴⁵ Yesu alifanya jambo lile lile. “Ni Neno; imeandikwa.” Naye Shetani akajaribu ku—kulifunika—funika, si kunukuu; kulifunika—funika kwa ajili Yake. Kisha Yesu akasema, “Na pia imeandikwa.” Sasa, hatuna budi kukaa na hilo Neno!

⁴⁶ Na katika kambi hii ndogo waliyokuwa nayo kule, ya Petro, Yakobo, na Yohana; na Yesu, Musa, na Eliya. Na katika kambi yao waliona jeshi la Mbinguni la kivuli, ama Nguzo ya Nuru ikining’inia katika wingu hili ambalo lilimgeuza Bwana Yesu. Na walipokuwa tayari kufanya madhehebu, moja kwa ajili ya torati, moja kwa ajili ya manabii, na kadhalika, Ile Sauti ikasema, “Huyu ni Mwanangu, Mpendwa Wangu; msikieni Yeye.” Kisha, kwa yale waliyoagizwa, ilikuwa tu hasa kama ilivyokuwa katika Edeni, “Dumuni na Neno!” Hiyo ndiyo kambi ya Mungu kwa ajili ya watu Wake.

47 Inaonekana, leo, kuwa siku ambayo watu wanaenda nje ya kambi. Katika kila kitu, wanapita mpaka.

48 Mnajua, niliambiwa, wakati fulani uliopita, ya kwamba wana ndege ambayo sasa inaweza...kufanya kelele hizo tunazosikia humu, ambazo hutikisa madirisha. Ni wakati ndege imeenda kasi sana hata inavuka sauti yake yenyewe, inaitwa kizuizi cha sauti. Na wakati inapita kizuizi chake cha sauti, yale itakayofanya karibu hayapimiki.

Nami nafikiri kwamba, ndani mle, tunapata somo. Tunapoenda nje ya kizuzi chetu cha sauti zetu, tukaingia katika Neno la Mungu, basi hayapimiki yale Mungu anayoweza kufanya na mtu ambaye yuko tayari kwenda nje ya kambi, kambi ya mwanadamu, hasa. Sasa, tunaona jambo hilo, kwenda nje ya kambi, kwenda nje ya hii.

49 Namwona Shetani, pia, anawachukua watu wake nje ya kambi ya hoja, nje ya—ya—ya kambi ya—ya akili ya kawaida. Shetani akiwachukua watu wake njia hii nyingine, nje ya kambi; Mungu akiwapeleka watu Wake nje, njia hiyo nyingine. Naye Shetani amewapeleka nje ya kambi ya uadilifu wa kawaida. Inapofikia mahali ambapo watu...na wanaweza kutenda na kufanya, na kuachiliwa kufanya mambo wanayofanya katika uadilifu. Sielewi kabisa jinsi mtu anavyoweza kumweka mke wake kule nje, amevalia namna hiyo, halafu ampige mtu kofi kwa kumtukana. Inapita akili za kawaida. Inampasa kujua vema zaidi ya hayo. Nje ya uadilifu wa kawaida! Mwisho wake ni wapi?

50 Baadhi yenu wanaume na wanawake wa umri wangu, huenda nikawauliza jambo hili. Vipi kama mama yangu au mama yako, yapata miaka hamsini iliyopita, alitoka akaenda kutembea barabarani na moja ya hizi kaptura ama bikini, sijui mnaziitaje, amezivaa? Sheria ingaliwashika, mara moja, na kuwaweka katika hospitali ya wenda wazimu. Bibi fulani alitoka nyumbani kwake kifua wazi, na anapaswa kupelekwa hospitalini, kwa maana hana akili timamu. Na kama ilikuwa wazimu kufanya jambo kama hilo wakati huo, bila shaka ni ishara kwamba kitu fulani kimepata wazimu. Ingali bado ni kupungukiwa na akili, mnaona, kurukwa na akili; uchafu!

51 Na wakati mtu anaweza kuvuta sigara, na huku madaktari wanamthibitishia ya kwamba maelfu wanakufa kila mwaka kwa sababu hiyo, na bado anaweza kuvuta sigara, inaonekana kwamba bongo la mtu huyo lina kasoro.

Na wakati mtu anapokuwa na mshtuko wa akili, na yeye ha-...hawezi kujimudu, anayofanya, atatafuta katika kila afisi ya daktari iliyopo nchini, kuona ana tatizo gani. Bali hata hivyo atasimama kwenye baa ama katika gari, na anywe mpaka amekuwa kichaa kabisa; atumie fedha zake, ili kujisukumiza humo ndani. Na ikitokea kwamba anaingilia jambo hilo bila

kulewa pombe, ndipo atatumia kila hela atakayopata, katika afisi ya daktari, akijaribu kuona ana tatizo gani. Haina maana.

⁵² Kama angalitokea mwewe mla kuku akiruka juu ya mji, nami nigechukua bunduki yangu, niondoke niende nyuma ya nyumba yangu na kumpiga risasi huyu mwewe, dakika kumi tokea hapo ningekuwa jela. Wangenishika, “Kwa—kwa kufanya ghasia; kutumia bunduki mjini; kuyahatarisha maisha ya watu, kwa bunduki, kumtupia mwewe risasi hewani.” Huenda nikamuua mtu, ndivyo wangesema. “Anapaswa kuondolewa mbali.”

Halafu watamuuzia mtu pombe ya kutosha hata akalewa, na kumwingiza kwenye gari ambalo laweza likaua jamaa nzima. Na anaposhikwa, atatozwa, dola tano za kugharimia kesi. Mauaji ya kudhamiria! Ulimwengu una nini? Kuna kasoro mahali fulani.

⁵³ Sasa, “kwenda nje ya kambi,” nje ya uadilifu, bila kutumia akili.

Mnaona, wanasiasa wetu hawatasema neno kuhusu kusoma Biblia shuleni. Wanahofu. Hawajui upepo unakoelekea. Hawajui kama watapoteza kura, au la. Tunahitaji Abraham Lincoln mwingine. Tunahitaji John Quincy Adam mwingine. Tunahitaji mtu fulani ambaye atasimama, haidhuru upepo unaelekea wapi, na kutoa wanayosadiki kwa uaminifu.

⁵⁴ Leo, mhubiri wa kimadhehebu, hata umwonyeshe katika Neno, ile Kweli, hajui la kufanya. Anaogopa atapoteza riziki yake. Tunahitaji wanaume na wanawake leo ambao ni mashujaa wa Injili, mtu ambaye atasimama na kusema wanayoamini, kuonyesha mabaya na mazuri, kama Neno la Mungu ni kweli au madhehebu ni kweli.

⁵⁵ Yesu alisema, “Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe Kweli. Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita.”

⁵⁶ Kwa hiyo, unaona, wao wanaenda nje ya kambi ya Neno la Mungu, kutafuta jawabu lao. Tunahitaji...Kile kimewashawishi watoke kambi ya Neno la Mungu, kama alivyomfanyia Hawa katika bustani ya Edeni, Shetani amefanya jambo lile lile leo. Vema. Tunaona hivyo. Watu wanashawishika na mafundisho yao ya sharti na kanuni za imani nje ya kambi, katika kambi yao ya mafundisho ya sharti na kanuni za imani. Wao wana kambi, pia, na hiyo inawaweka katika kambi yake. Kambi yake ni kambi ya elimu, theolojia, kazi, shahada za udaktari, kielimu, utu, kila kitu ambacho ni kinyume cha kambi ya Neno la Mungu. Mungu yuna kambi kwa ajili ya watu Wake. Madhehebu yana kambi zao.

⁵⁷ Miaka mia tatu iliyopita, mtu angeweza kukutana na Mungu karibu kila mahali. Ilikuwa jambo la kawaida kwa mwanadamu kukutana na Mungu. Lakini mbona hawakutani Naye leo? Kuna watu wengi zaidi, maelfu mara maelfu na mamilioni ya watu

wengi zaidi kuliko waliokuweco miaka elfu tatu iliyopita, na hata hivyo Mungu ni kitu fulani cha kale kilichozungumzwa, historia fulani ya kale. Wao hawakutani na Mungu, uso kwa uso, kama walivyofanya miaka mingi iliyopita, kama nilivyosema, elfu tatu, yapata miaka elfu tatu iliyopita. Hawakutani. Si jambo la kawaida kwa mtu kukutana na Mungu. Kama mtu akizungumza juu yake, anadhaniwa ana kichaa, mtu ambaye hana akili. Ni jambo lisilo la kawaida sana kwao!

⁵⁸ Kwa habari ya Ibrahimu na katika kambi yake, mbona, lilikuwa jambo la karibu kila siku kwa Ibrahimu kukutana na Mungu. Yeye alizungumza Naye. Si hivyo tu, bali waliposhuka wakaenda Gerari, kama wageni; tunaona, kule chini, ya kwamba Mungu alikuwa kambini pamoja na Abimeleki, Mfilisti. Lilikuwa jambo la kawaida sana. Wao waliishi katika kambi ya Uwepo Wake.

Leo, wanaishi katika kambi yao wenyewe, na hawana uhusiano wo wote na kambi ya Mungu. Hawataki uhusiano wo wote nayo, kwa sababu ni ushupavu wa dini kwa ulimwengu. Ni ushupavu wa dini kwao. Bali, kumbuka, wakati Mungu alipofanya kambi ya kwanza kwa ajili ya watu, Yeye aliwafanyia ngome kwa Neno Lake. Yeye daima hufanya hivyo. Bali, leo, katika kambi zao, hawafanyi hivyo. Hiyo ndiyo sababu husikii mengi sana juu ya Mungu. Sasa, naamini ya kwamba ile—kwamba ile kambi. . .

⁵⁹ Kama vile Musa, jinsi alivyokutana na Musa jangwani. Musa alikuwa na kambi kule nje alipokuwa akilisha kondoo za baba mkwe wake, Yethro, upande wa nyuma wa jangwa. Ndipo siku moja, kwa huyu mchungaji mwenye umri wa miaka themanini, aliona Nuru, Nguzo ya Moto katika kijiti, kikiwaka moto. Naye akakutana na Mungu; mtu aliyekuwa anamkimbia Mungu.

Siku iliyofuata. Wakati mwingine kukutana na Mungu hukufanya ufanye mambo yasiyo ya kawaida. Musa alikuwa mtu asiye wa kawaida sana, kesho yake. Alimketisha mkewe juu ya nyumbu, na mtoto mchanga amempakata kiunoni mwake; na ndevu zake ndefu zinaning'inia, fimbo iliyopinda mkononi mwake, akishuka kwenda Misri, kuliteka hilo taifa. Hilo lilikuwa tamasha kwelikweli.

“Unaenda wapi, Musa?”

“Naenda Misri.”

“Kufanya nini?”

⁶⁰ “Kuiteka!” Alikuwa tayari amekutana na Mungu. Uvamizi wa mtu mmoja. Lilionekana la kigeni sana. Lakini, jambo ni kwamba, alifaulu, kwa maana tayari alikuwa amekutana na Mungu. Ni kama tu mtu mmoja akienda kuiteka Urusi; hilo tu ndilo unalohitaji, mtu mmoja katika mapenzi ya Mungu. Musa alikuwa katika mapenzi ya Mungu. Na alikuwa na fimbo

iliyopinda mkononi mwake, si upanga; fimbo. Mambo yasiyo ya kawaida, huyafanya Mungu.

⁶¹ Lakini, kumbuka, ilimbidi Musa kutoka katika kambi alimokuwa anaishi, kufanya jambo hili, kwa sababu alikuwa kule chini na jeshi zima na hangeweza kufanya hivyo. Ingawa alikuwa na jeshi lote la Misri, hangeweza kufanya hivyo. Bali siku moja Mungu alimwalika kwenye kambi yake.

Akasema, “Wewe U nani?”

⁶² Akasema, “MIMI NIKO AMBAYE NIKO.” Si, “Nilikuwa, ama nitakuwa.” Wakati uliopo, “MIMI NIKO! Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa Yakobo. Nimesikia kilio cha hao watu, Nami ninakumbuka ahadi Yangu, na huu ndio wakati wa haya kutimizwa. Mimi ninakutuma ushuke uende kule, Musa, na fimbo hii iliyo mkononi mwako.”

⁶³ Ilikuwa nini? Yeye, sasa, watu walifikiri alikuwa na kichaa. Bali alikuwa amefanya nini? Alitoka kwenye kambi yake. Farao alimwelimisha kwa miaka arobaini katika kambi ya shule, naye akashindwa. Ndipo ikamchukua Mungu miaka mingine arobaini kuitoa ndani yake. Elimu yake yote na theolojia yake ambayo alikuwa amefundishwa, ilichukua miaka arobaini kuitoa ndani yake. Ndipo Mungu akamtumia miaka arobaini.

⁶⁴ Mungu huwa na wakati mgumu sana anapomtayarisha mtu Wake. Lakini, unaona, Yeye kamwe hangeweza kumshika Mus-... kumshika Musa, hata Musa alipotoka kwenye kambi yake ya kujitengenezea, akatoka kwenye kulitenda hilo kwa njia ya kijeshi, na kulitenda kwa njia ya kiasili, hata akafikia kulitenda jambo hilo kwa njia ya kimbinguni. Ndipo, wakati alipofika katika kambi hiyo, Mungu alieweza kumtumia.

⁶⁵ Sasa, tunaona ya kwamba katika jangwa hili... Tunaona wakati walishika na kuchukua msimamo wao, na wakatoka Misri, wakaingia kwenye kambi ya Mungu; kutoka kwenye kambi za makuhani na hao wote waliokuwa wakisema, “Jiuzeni kama watumwa, kwa muda uliosalia.” Wakati nabii Musa aliposhuka na kuthibitisha kwamba Neno la Mungu lilikuwa limewadia, ya kwamba Mungu aliyefanya ile ahadi alikuwa pale kuwakomboa hao watu; walitoka kwenye kambi walimokuwemo, wakaingia kwenye kambi ya Neno la Mungu lililoahidiwa la wakati huo. Wao walimwamini huyo nabii, kwa sababu ile ishara ya kuthibitisha ilikuwa ikithibitisha ya kwamba lilikuwa Neno la Mungu hasa. Na mambo aliyofanya yalithibitisha ya kwamba lilikuwa ni kweli, na ile Nguzo ya Moto ilimfuata, ikithibitisha kwamba ilikuwa Neno la Mungu.

⁶⁶ Sasa, katika kambi hii, miujiza, ishara, maajabu yalikuwa katika kambi hii.

Waliwatoa wakawapeleka jangwani. Waliiacha kambi yao ya kiasili. Wakaacha kambi yao ya matope. Waliiacha kambi yao iliyojengwa kwa majani makavu na matofali, wakaishi

katika hema jangwani, pasipokuwa na nafaka ama cho chote kile. Wakati mwingine Mungu hutuagiza kutenda mambo ya kipumbavu, kwa mafikara yetu. Na kama ukiwahi kuiacha kambi ya hoja zako, hapo ndipo mahali utakapompata Mungu.

⁶⁷ Angalia, walipotoka kwenda jangwani, kulikuwa na miujiza, ishara, walipoingia katika kambi hii. Sasa kumbukeni, waliacha kambi ya Misri wa kaen da i a n awani na kambi ya Mungu. Unajuaje ilikuwa hivyo? Mungu alisema, “Watu wako watakuwa wageni kwa miaka mia nne, bali nitawatoa kwa mkono wenye nguvu, nami nitawapa nchi hii hapa.” Nao walikuwa wameshika njia, kwa Nuru iliyothibitishwa, nabii aliyethibitishwa, kwa ishara, maaajabu, ya kwamba Mungu alikuwa katika kambi, nao walikuwa wakienda zao. Walikuwa na Nguzo ya Moto. Walikuwa na nabii. Walikuwa na mana. Walikuwa na maji yaliyo hai. Amina! Walikuwa wamebadilisha, wamebadilisha mahali pa kupiga kam bi. Iliwabidi kufanya hivyo. Hawakuweza kuyaona mambo hayo huko Misri. Iliwabidi kubadilisha mahali pa kupiga kambi, wapate kuona ya kimbinguni.

⁶⁸ Vi vyo hivyo itawabidi watu wa siku hizi kubadilisha kambi kutoka kwa madhehebu yasemayo, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na Maandiko haya yote yamekosea; nayo ni ya wakati mwingine.” Huna budi kubadilisha mahali pako pa kupiga kambi, nenda nje ya kambi hiyo, hata kwenye mahali ambapo yote yawezekana.

⁶⁹ Yote yalikuwa yakithibitisha Uwepo Wake kambini. Sasa angalia basi, hao, walikuwa wamefanya kambi ya kujitengenezea ya mapokeo na kanuni ya imani, baada ya kufa kwa Musa. Naye Mungu akawashughulikia hao watu kwa miaka mingi. Mungu hayuko katika kambi Yake, tena, katika kambi yao, kwa sababu walijifanyia kambi, kambi ya kujifanyia wenyewe.

⁷⁰ Kumbukeni, walipoitwa kutoka Misri, Mungu aliwapa nabii, akawapa mwana-kondoo wa sadaka, akawapa yote waliyohitaji; neno, ishara, miujiza, nabii wa kuwaongoza, upatanisho wa kuwashughulikia, Nguzo ya Moto kuwaongoza. Nao walipofika jangwani, bado hawakuridhika. Walitaka jambo la kufanya, wao wenyewe. Neema ilikuwa imetoa hayo; sasa wao wanataka jambo la kufanya, wao wenyewe, kusudi wajiundie madhehebu, na kugombana na kupigana na kuzozana, ni nani atakuwa kuhani mkuu, na ni nani atakuwa *hiki*, *kile*, au *kingine*. Siku moja, Mungu akasema, “Musa, jitenge nao,” Naye akawameza tu katika maasi ya Kora.

⁷¹ Sasa tazama, ishara hizi zote na maajabu vilithibitisha Uwepo Wake.

Ndipo akajitengenezea, mwanadamu akajitengenezea kambi, kambi ya kanuni ya imani na mapokeo, si kambi ya Mungu ya Neno Lake. Kambi yao wenyewe! Ilimbidi kuwaacha,

kwa maana Yeye ni Neno. Yeye hawezi kukaa mahali ambapo watu wanafundishwa nje ya Neno hili. Mungu hawezi kukaa kambini. Hawezi. Hajafanya hivyo kamwe. Yeye hana budi kukaa mahali lilipo Neno Lake.

⁷² Ilipompasa kuacha hiyo kambi, basi, ya kundi hilo lote la watu alilolipandisha kutoka Misri, alikaa tu kati ya manabii wake, ambao walijiliwa na Neno Lake. Neno lilimjia nabii, kuthibitisha huo wakati. Yeye aliishi miongoni mwa manabii, na kufunuliwa kwa nabii. Jinsi walivyolaani, hao watu, na kulaani kitu hicho. Kisha Mungu akawafundisha amri Zake na njia ya maisha. Nao watu daima walikuwa wanaipinga, na kumtesa nabii, na hatimaye wakampiga mawe, ama kumkata kwa msumeno vipande-vipande, wakamwondolea mbali.

⁷³ Yesu alisema, “Ni yupi kati ya manabii ambaye baba zenu hawakumuua? Ni yupi miongoni mwao, kati ya wale wenye haki waliotumwa kwao?” Kisha kasema, “Kazi za baba yenu mtazifanya.” Hakuwa akiwazungumzia wakomunisti. Alikuwa akiwazungumzia makuhani, watu wa kimadhehebu, Mafarisayo na Masadukayo. Nadhani sauti Yake haingebadilika sana usiku wa leo, ila itakakuwa mbaya zaidi, labda, kwao.

⁷⁴ Sasa, tunaona ya kwamba alikaa miongoni mwa manabii Zake. Ndipo akawa mgeni kwao, kwa kuwa Yeye hudumu katika Neno Lake tu, kulithibitisha. Biblia ilisema ya kwamba Yeye hulilinda Neno Lake, apate kulithibitisha. Yeye anajaribu kumpata mtu fulani.

Kama tu anaweza kumpata mtu kigeugeu, kama Samsoni. Samsoni alisalimisha nguvu zake kwa Mungu, bali akampa Delila moyo wake. Hivyo ndivyo tunavyofanya mara nyingi, leo, tunampa tu Mungu kitu fulani, bali si yote. Lakini, Mungu anahitaji yote, yaliyo yetu.

⁷⁵ Ni kama bima, unapopata bima, afadhali uichukue yote. Na hivyo ndivyo hii dhamana yenye heri inavyotufanyia. Ni bima nzima. Inashughulikia yote tunayohitaji katika maisha haya, na kufufuka kwetu, na Uzima wa Milele. Inahusika na mambo yote.

⁷⁶ Angalia, Mungu alikaa nje ya kambi yao kwa miaka mia nne. Kwa nini? Hakuwa na manabii wengine. Tangu nabii Malaki, hata nabii Yohana, miaka mia nne, hakuna hatua hata moja waliyopiga Israeli. Mungu alikuwa nje ya kambi. Wao walimweka nje, kwa kanuni zao za imani na uchoyo wao, na tofauti zao kwa Neno. Miaka mia nne bila Neno! Kutoka nabii mmoja hadi mwingine, Yeye alisafiri, hata nabii wa mwisho alikuwa Malaki, ndipo hapakuwepo na nabii mwingine kwa miaka mia nne.

⁷⁷ Ndipo Mungu akajitokeza tena. Siku moja Yeye akatembea miongoni mwao tena, bali mapokeo yao yalikuwa yamepachukua mahali Pake sana miongoni mwao, alikuwa mgeni kwao. Mapokeo ya baba zao, walikuwa na kusafisha

vyombo, na—na jinsi ya kutengeneza nywele zao, na kutia vifungo fulani kwenye makoti yao, na majoho ya makuhani—ya makuhani; na mmoja ni Mfarisayo shupavu, na mwingine ni Msadukayo. Na jambo hilo lilikuwa limepachukua mahali pa Neno miongoni mwa hao watu, hata, Mungu alipowazuru, alikuwa mgeni.

⁷⁸ Hebu niseme jambo hili kwa upendo na heshima, lakini kulisisitiza. Ni jambo lilo hilo leo hii. Haijabadilika hata kidogo. Wakati anapokuja miongoni mwa watu, katika nguvu Zake na dhihirisho, kuthibitisha kwamba Neno Lake ni lile lile jana, leo, na hata milele, maana Yeye ni Neno, watu wanasema, “Mpiga ramli, Beelzebuli, Yesu pekee, au—au kitu kama hicho.” Baadhi yao wanakuweka katika kundi fulani, lakini haina budi kuwa namna hiyo.

Mnaona, hatujakuwa na nabii sasa kwa karibu miaka elfu mbili. Mataifa hawakumpata mmoja, mwajua; ameahidiwa mwishoni. Sasa, tunajua jambo hilo, kwa Maandiko. Tunajua jambo hilo, pia, kwa historia ya kwamba tumeahidiwa jambo hili.

⁷⁹ Sasa, baada ya miaka mia nne, Mungu alitembea moja kwa moja miongoni mwao siku moja. Kulingana na Maandiko, Yeye alikuwa afanyike mwili na akae miongoni mwao. “Jina Lake ataitwa Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye Nguvu, Baba wa Milele.”

Na wakati alipokuja miongoni mwa watu, wao walisema, “Hatutaki Mtu huyu atutawale! Ana—ana kadi gani ya ushirika? Alitumwa na madhehebu gani?” Hakuungwa mkono. Kila kanisa aliloliendea, walimtupa nje. Hawakuwa na uhusiano wote Naye, kwa kuwa hakuwa mmoja wao.

Na kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo leo! Biblia ilisema kanisa la Laodikia lingemtupa nje, Naye alikuwa anabisha, akijaribu kuingia. Kuna kasoro mahali fulani.

⁸⁰ Sasa, kwa nini? Walikuwa wamefanya kambi yao wenyewe. Wao, kama wangelikuwa wamejua Neno, wangelijua Yeye alikuwa nani. Yesu alisema, “Kama mki-... Yachunguzeni Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake. Hayo ndiyo yanayowaambieni Mimi ni Nani!” Hivyo ndivyo yalivyosema Maandiko. Sasa, “Yanashuhudia Mimi. Na kama sizitendi kazi zilizoahidiwa kutendwa Nami, kama sizitendi kazi za Baba Yangu, Neno... ‘Hapo mwanzo alikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.’ Sasa, kama Mimi ndiye Mtu huyo, yachunguzeni Maandiko muone ninalopaswa kutenda. Na iwapo Mimi sina sifa hizo; iwapo kazi Zangu, kazi ambazo Neno linashuhudia, Baba hunishuhudia Mimi, kama hizo hazithibitishi Mimi ni Nani, basi

nimekosea.” Hiyo ni kweli. “Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini Neno,” Yeye alisema, “kazi ambazo Neno linatenda.”

⁸¹ Mnaona, Yeye alikuwa mgeni kati yao. Wao hawakumjua. “Hatumtaki Mtu huyu, Mtu wa kipekee tu aliyezaliwa kule chini horini mahali fulani.” Nao waliamini ya kwamba mamaye alimpata Mtoto huyu kabla hajazaliwa, ama kabla haja... alimpata Mtoto huyu kwa njia haramu, hasa. Halafu, wao, kwamba kabla Mtoto huyu hajazaliwa, ya kwamba aliondoka akaenda akaolewa na Yusufu; naye eti alifanya hivyo tu ili kujiondolea lawama, tabia yake. “Ndipo akawa Mtu wa kipekee, kwa maana alizaliwa mwana haramu, na hiyo ndiyo sababu Yeye alikuwa hivyo.”

Naye alipotoka, alifanya nini? Akararua kanuni zao za imani, akapindua meza zao, akawapiga akawatoa mahali pale, na kusema, “Imeandikwa!” Amina! [Ndugu Branham anapiga makofi mara nne—Mh.] Hilo lilipaswa kuwaambia Yeye alikuwa Nani. “Imeandikwa!”

⁸² Vema, hao hawangejijhusisha na Jamaa kama huyo. Bali katika kilindi cha mioyo yao, wao walijua alikuwa Nani, kwa maana Nikodemo alinena hayo dhahiri: “Rabi, sisi, Mafarisayo, tunajua Wewe ni mwalimu aliyetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna Mtu awezaye kufanya mambo ufanyayo Wewe isipokuwa Mungu yu pamoja Naye.” Kwa nini hawakumkiri basi? Ni kwa sababu kambi yao ilikuwa imeweka mpaka wake. Haingemruhusu kambini. Haingemruhusu mtu ye yote aende Kwake. Walikuwa na kambi yao wenyewe. Alikuwa usiku, wakati lango lilikuwa limefungwa kwelikweli. Lakini aliona kwamba angeweza akakutana Naye, hata hivyo.

⁸³ Ndiyo, jambo lilo hilo sasa! Wanayo... Yeye amekuwa mgeni, mtu wa nchi nyingine. Hawaelewi Hilo. “Mbona iwe *hivi*, na mbona vile?” Wakati, Neno lenyewe linashuhudia ya kwamba hivi ndivyo inavyopaswa kufanywa hasa katika siku hii. Jinsi tulivyopitia jambo hilo, tukalirudiarudia, bali ni Kweli.

⁸⁴ Alikuwa, kwa hao kambini mwao, “Shupavu wa dini, mvunja mapokeo yao, mvuruga makanisa yao, kwa kweli ni mpiga ramli tu, mwabudu mizimu anayeitwa ‘Beelzebuli.’ Hivyo ndivyo alivyokuwa.”

Nami naamini, kama akija miongoni mwetu leo, angekuwa jambo lile lile, kwetu sisi. Kwa kuwa, tuna mapokeo, tuna madhehebu, hata hatuwezi kuvumiliana. Kwa nini? Kuna mahali pamoja tu ambapo mtu anaweza kushiriki, hapo ni, chini ya Damu iliyomwagwa. Nayo Damu ilimwagwa, kama chembechembe ya uhai, kuchipusha hii Mbegu, Neno. Nje ya hayo, vizuizi vyetu vya kimadhehebu daima vitawaweka watu nje.

⁸⁵ Lakini angekuwa mgeni leo. Angeitwa kitu kile kile. Angetendewa, angetolewa kambini. Na mlijua... Biblia ile

ile iliyosema angekataliwa na wanadamu, “Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko,” nao wakakataa, “na tulimdhania ya kuwa amepigwa, na kuteswa na Mungu,” Maandiko yale yale yaliyosema hayo. Nabii yule yule aliyeimba, “Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Mifupa Yangu, wote wananikodolea macho. Wamenizua mikono na miguu Yangu.” Wakati walipokuwa wakiimba huo wimbo kanisani mwao; Dhabihu yao, Mungu yule waliyemdhania wanamtumikia, walikuwa wanamsulubisha.

Ndivyo ilivyo leo, Mungu yule yule!

⁸⁶ Angalia aliyosema nabii, Amosi, alipofika Samaria. Na macho yake madogo yakarudiana alipopanda akaja kule na kuuona huo mji wenye dhambi, wanawake wamelala barabarani, na wanaume, Marekani ya kisasa. Alipouangalia, macho yake yakarudiana. Naye hakuwa na wa kumdhamini. Hakuwa na kadi ya ushirika. Mungu alikuwa amemtuma. Je, watu wangesikia Ujumbe wake? La, hawangemsikia. Bali alitabiri, akasema, “Mungu yule yule mnyedai mnamtumikia atawaangamiza.”

Nami nasema, katika Jina la Yesu Kristo! Mungu yule yule taifa hili linadai kuwa, taifa la kidini, Mungu yule yule wanayedai wanamwabudu atawaangamiza katika uovu wao. Yeye ataangamiza kila madhehebu kutoka kwenye uso wa dunia, ambaye wanadai kumtumikia.

⁸⁷ Kwa hiyo, angalia, Yeye aliwakemea, nao wakamfukuza kambini mwao. “Yesu aliteswa nje ya kambi.” Walimfukuza nje ya kambi yao, nje, mbali sana na kambi yao.

⁸⁸ Tunaona ya kwamba Biblia ilisema, katika siku hizi za mwisho chini ya huu Wakati wa Laodikia, wangefanya jambo lile lile. Wao wangewekwa nje ya kambi.

Sasa tazama anachosema kifanywe sasa, katika kufunga.

“Katupwa nje ya kambi,” ambapo dhabihu ziliteketezwa. Hapo ndipo palikuwa mahali Pake. Yeye alikuwa ile Dhabihu.

⁸⁹ Sasa, ndugu, dada, mnajua ya kwamba kila mmoja wenu hana budi kujitoa dhabihu? Huna budi kuwa dhabihu ya Mungu; ujinyime mambo ya ulimwengu, ujinyime anasa zako za ulimwengu huu, ujinyime mambo ya ulimwengu? Unajua sababu watu hawatafanya hivyo?

⁹⁰ Mnajua, kondoo, kondoo hana ila kitu kimoja cha kutoa, na hicho ni sufu. Na, sasa, yeye haombwi kutoa ama kutengeneza sufu kwa mwaka huu. Yeye anaombwa kutoa . . . kuzaa sufu.

Sisi hatuombwi kutengeneza kitu fulani. Tunaombwa kuzaa matunda ya Roho. Yaani, ndani ya kondoo, kile alichu kwa ndani, kinafanya sufu kwa nje. Na wakati mtu ana Kristo kwa ndani, inamfanya kama Kristo kwa nje, si kitu cha kujitengeneza.

⁹¹ Vema, tunaona jambo hilo linapotukia, Kristo anaporudi, Yeye anafanyiwaje? Ni kama tu vile alivyokuwa hapo mwanzo. Imekuwa hivyo daima.

⁹² Kwa hiyo, Yeye aliwakemea sana, hata wakawatoa nje ya kambi Yake, na kumfanya mwenye dhambi. Ambalo, “Yeye alifanyika dhambi kwa ajili yetu.”

⁹³ Sasa, baada ya mamia ya miaka, ndiyo, karibu miaka elfu mbili, ameizuru kambi yao tena, kulingana na Neno Lake lililoahidiwa ya kwamba atafanya hivyo katika siku za mwisho. Yeye ameizuru kambi tena. Yeye ameizuru kambi, kudhihirisha Neno hili leo.

Kama tu alivyoizuru katika siku hiyo, na akafanya katika siku za Musa. Hiyo haikuwa Musa akifanya hivyo; Musa alikuwa mwanadamu. Ilikuwa ni Kristo.

⁹⁴ Mwangelie Yusufu, yale maisha; alipendwa na babaye, akachukiwa na nduguze, kwa maana alikuwa mwonaji. Nao walimchukia, bila sababu. Hiyo ndiyo tu iliyokuwa sababu ya kumchukia.

Mfano mkamilifu wa siku hizi, hasa. Kanisa, tena, wanachukia mambo ya kiroho.

Nasi tunaona kwamba aliuzwa kwa yapata vipande thelathini vya fedha, akidhaniwa alikuwa amekufa. Akachukuliwa akawekwa gerezeni; kama ilivyotukia kwa Yesu msalabani. Mtu mmoja alipotea, mtu mmoja akaokolewa; naye aliondolewa pale akawekwa mkono wa kuume wa Farao. Hivyo ndivyo Yesu alivyofanywa hasa.

⁹⁵ Ilikuwa Daudi, naye akapita mitaani, akilia, mfalme aliyekataliwa; akaketi mlimani, akililia Yerusalemu. Huyu hakuwa Daudi. Mwana wa Daudi, miaka mia kadha baadaye, aliketi kwenye kilima kile kile akalia kwa maana Yeye alikuwa Mfalme aliyekataliwa miongoni mwa watu Wake Mwenyewe. Ni Kristo, daima.

Na, leo, wakati imetabiriwa ya kwamba Kristo hana budi kuja kambi, unajua kilichotukia? Itakuwa sawa kabisa kama ilivyokuwa wakati ule. Haina budi kuwa namna hiyo, kutimiza kile Neno hapa lilisema atafanya.

⁹⁶ Sasa kumbuka, Kristo alikuwa katika wakati wa Nuhu. Huyu alikuwa ni Kristo, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele,” Neno lililokataliwa la wakati huo.

⁹⁷ Angalia, na unabii Wake wa Ufunuo 3, tuliona, alipokuja katika siku hii ya mwisho, kama alivyotabiri atakuja katika siku hii ya mwisho. Naye alilikutaje kanisa wakati Laodikia? “Tajiri, halina haja ya kitu.” “Na limeketi malkia na haliwezi kuona huzuni kamwe.” “Na kumweka nje ya kanisa,” hakuwafaa kitu. Akatoka nje ya kambi tena. Lakini basi halikuja ya kwamba lilikuwa uchi, kipofu, na lenye mashaka; na halikuja.

⁹⁸ Tena, kama akija tena kwa njia ile ile aliyokuja wakati huo, Yeye angemkemea kila mwanamke aliyevaa kaptura. Angemkemea kila mwanamke aliyekata nywele zake, kila uso uliopodolewa, kila mwanamume ambaye angekuwa duni kutosha kumwacha mkewe afanye hivyo. Bado angefanya hivyo. Halafu angeyararua kila madhehebu yaliyokuwepo, na kuvunja kila kanuni ya imani tuliyoukuwa nayo. Mnaamini angefanya hivyo? [Kusanyiko, “Amina! —Mh.] Bila shaka angefanya hivyo. Hiyo ni kweli.

⁹⁹ Wao wangemfanyaje? Wangemtoa nje ya kambi. Bila shaka hawangeshirikiana Naye. La, bwana!

¹⁰⁰ Sasa tunamwona tena, katika siku hii, kama Biblia ilivyosema angefanya, ametupwa nje ya kambi. Kwa maana Yeye daima hudumu yeye yule, Neno, yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁰¹ Wao—wao hawamtaki. Walimkataa tena, pamoja na halmashauri yao. Wangetaka, leo, kama walivyofanya wakati huo wakati Yeye alipokuwa anashtakiwa. Na leo, wakati Neno linashtakiwa, kumetukia nini? Wamemkataa tena kama walivyofanya wakati huo, na kumkubali Baraba, muuaji, badala ya Kristo. Halmashauri ingefanya jambo lile lile. Na, leo, kwa sababu wamelikataa Neno na thibitisho halisi la saa hii, wamemsaliti kisha wakampendelea Baraba, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, muuaji wa Neno. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁰² Wao wanalikana Neno Lake, wanaukana ubatizo, wanakana Nguvu Zake, na kuzikana ishara Zake. Na kwa kanuni za imani ama mapokeo tena, ya kuvalia kosi zilizopinduliwa, na kila kitu, wakijifanyia kanuni za imani, na kadhalika, wanajaribu kufanya hivyo, kwa matendo mema. Wao hawakuchaguliwa wapate Uzima, kwanza. Hawakuwa na cha kuaminia.

“Yeye anijuaye Mimi, anamjua Baba Yangu. Na kama Baba alivyomituma Mimi, Mimi Nami nawapeleka ninyi.” Mungu aliyemituma Yesu aliingia ndani ya Yesu. Na Yesu anayekutuma anaingia ndani yako. “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe,” cheusi, cha kimanjano, cheupe, cha hudhurungi, cho chote kile. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mbona umbali gani? “Ulimwenguni kote, na kwa kila kiumbe.”

¹⁰³ Maskini mhudumu wa Kibatisti, si muda mrefu uliopita huko Tucson, alinjia, kasema, “Ndugu Branham, shida yako iko hapa. Unajaribu kuufanya huu kuwa wakati wa kimitume.” Akasema, “Hakuna kitu kama wakati wa kimitume leo. Wakati wa kimitume umekwisha.”

¹⁰⁴ Nikasema, “Ati umekwisha? Sikujua.”

Kisha akasema, “Vema, umekwisha.”

Nikasema, “Una hakika?”

Akasema, “Hakika. Nina hakika,” akasema.

“Sawa,” nikasema, “unafikiri umeishaje?”

Akasema, “Huo ulikuwa kwa ajili ya wale mitume.”

¹⁰⁵ Nikasema, “Petro alisema, katika Siku ya Pentekoste. Unaamini Neno lake?”

“Naam, bwana.”

¹⁰⁶ “Yeye alisema, ‘Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watoto wa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.’”

¹⁰⁷ Ahadi ii hii, hatuna budi kuirudia! [Ndugu Branham anagonga mimbarani—Mh.] Daktari Simoni Petro aliandika maagizo. Biblia ilisema, “Je! hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu?”

Vema, mnajua, kama ukichukua maagizo ya daktari. Wakati anapoupata ugonjwa ulioko ndani ya mwili wako, naye anaandika maagizo hayo; afadhali uyatimize, umtafute muuza dawa halisi ambaye atayatimiza vile vile tu ilivyoandikwa. Kwa maana, hana budi kutia sumu kiasi fulani, na dawa ya kuharibu nguvu ya sumu kiasi fulani, kiasi ambacho mwili wako utakimudu. Unaona, yeye... Tayari imejaribiwa na kuhakikishwa, nawe huna budi kuchukua maagizo hayo. Kama huyachukui, nawe umwache daktari bandia kuchezea hayo, ambaye hajui jinsi ya kuipima hiyo dawa ipasavyo, atakuua. Na kama akitia isiyo na nguvu mle, haitakufaa kitu.

¹⁰⁸ Na hiyo ndiyo shida ya wengi wenu enyi madaktari. [Ndugu Branham anagonga mimbarani—Mh.] Mnayachezea hayo maagizo!

Petro alisema, “Nitawapa maagizo ya milele, kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Si ati, “Njoo ukajiunge.” Lakini, “Tubuni, kila mmoja wenu, makabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea matokeo,” amina, “Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii, maagizo haya, ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu.”

Sasa, baadhi yenu ninyi madaktari bandia, acheni kuandika hayo maagizo ya bandia. Mnaona? Mnawaua watu wenu. A-ha. Hiyo ndiyo sababu kile Kitu halisi hakiwafikii. Ndiyo.

¹⁰⁹ Mnajua, katika maagizo yaya haya, jinsi daktari anavyopata dawa yake. Wao daima huchukua halafu... Wanasayansi wanajaribu kukisia kitu fulani, halafu wanakipa kijinguruwe, waone kama kitamuua ama la.

Kisha, mwajua, dawa, ni pata potea. Wewe, huenda ukapata afya, na huenda ikakuua, unaona, kwa maana watu wote si kama vijinguruwe, labda.

Kwa hiyo, basi kuna kitu kimoja kuhusu maagizo haya, ni kwa wote.

¹¹⁰ Na, basi, daktari ye yote mzuri ambaye hat-...ana imani kubwa katika madawa yake, hatamuuliza mtu mwingine. Wengine wao ni waoga vya kutosha kumchukua mfungwa mwenye kifungo cha maisha, halafu wanamweka huru kama akiistahimili, wanamwacha achukue hayo maagizo.

¹¹¹ Lakini, hapa, tulikuwa na Daktari halisi. Yeye alikuja, akachukua hayo maagizo, Mwenyewe. Mnaona? “MIMI NIKO.” Si, “Nitakuwa.” “Mimi ndimi ufufuo na Uzima,” asema Mungu. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Naye kila aishiye na kuniadini hatakufa kabisa hata milele.” Martha akasema... Yeye akasema, “Je! unayasadiki hayo?”

¹¹² Akasema, “Naam, Bwana, nimesadiki ya kwamba Wewe Ndiwe Kristo yule ajaye ulimwenguni. Haidhuru wengine watakuita nini, mimi tayari nimeliona!”

¹¹³ Pale Kalvari, Yeye alidungwa sindano, Yeye Mwenyewe. Na katika asubuhi ya Pasaka, mauti hayangaliweza kumshikilia. “Mimi Ndimi ufufuo na Uzima.” Walimdunga mauti, bali alifufuka, akiwa mshindi juu ya mauti, kuzimu, na kaburi. Yeye alidungwa sindano, Yeye Mwenyewe.

Naye akawatuma madaktari kuandika maagizo, ambao walikuwa na ufunuo wa Yeye alikuwa nani.

“Watu husema Mimi Mwana wa Adamu ni Nani?”

¹¹⁴ Petro akasema, “Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

¹¹⁵ Yeye akasema, “Heri wewe, Simoni. Umelipata sasa. Nakupa wewe funguo za Ufalme. Lo lote ufungalo duniani, nitalifunga Mbinguni. Ukilifungua duniani, nitalifungua Mbinguni.”

¹¹⁶ Na katika Siku ya Pentekoste, walipoona haya yote yakiendelea, Yeye alisema...Wao walisema, “Tufanyeje tupate chanjo hii?”

¹¹⁷ Hapa akasoma yale maagizo. Akasema, “Sasa mimi nitaandika maagizo. Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

Usiyachezee hayo maagizo; utakufa! Wanayafanya hafifu sana, siku hizi, hata si kitu ila maji ya kimadhehebu, hiyo ni kweli, dawa fulani ya kuhifadhi maiti wanayomdunga mtu aliyekufa kumfanya awe mfu zaidi.

Loo, lakini, ndugu, kuna kutiwa mafuta halisi! Kuna...?...! Ni kwa ajili ya kuiponya nafsi. Hebu usiyachezee

hayo maagizo. Yachukue hayo maagizo jinsi tu yalivyoandikwa, naye Mungu anawajibika kwa Neno Lake; hawajibiki kwa kanuni ya imani, ama fundisho la sharti, ama madhehebu. Yeye anawajibika kwa Neno Lake. Fuata hayo maagizo, huo ndio msingi wa kwanza. Anza, ndipo tayari umeruhusiwa na uko tayari kwenda kazini.

Tazama, “nje ya kambi.”

118 Wao wamemchagua Baraba leo. Wakati Injili imepita huku na huko, kila mahali ulimwenguni, ishara kuu na maajabu vimeufuata huo ufufuo, lakini, badala ya kuingia na kujaribu kulitekeleza hilo, wanaungana moja kwa moja na Baraba. “Kabla hatujakuwa na upuzi huu, na kadhalika, kanisani mwetu, tutakuwa wa tabaka bora kama wengine wao.” Sasa wana Rumi na hao wote pamoja, Baraba fulani. Tazama, basi sisi tuko katika kambi hiyo kuu.

119 Tumealikwa kwenda nje ya kambi hiyo. “Yesu pia, apate kuwatakasa watu kwa Damu Yake Mwenyewe, aliteswa nje ya lango. Basi tutoke tumwendee nje ya lango,” tazama, “tukichukua shutumu Lake.”

120 Alishutumiwa kwa jambo gani? Si kwa sababu alikuwa Mmethodisti au Mbatisti, nitawahakikishia jambo hilo; si kwa sababu alikuwa Mfarisayo ama Msadukayo. Kwa sababu alikuwa neno lililothibitishwa.

121 “Tukichukua shutumu Lake,” kwa (nini?) Neno lililothibitishwa. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo alivyofanya. Yeye alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba yangu, msiniamini; kama Mimi si jibu la maswali yote ya Biblia.”

122 Yesu wa Agano Jipya alikuwa Yehova wa la Kale. Kweli kabisa! Naamini, kama nilivyokuwa nikiwaambia hapa sasa, wakati fulani uliopita, ama mahali fulani mkutanoni. Huenda isiwe hapa. “Yehova wa Agano la Kale Ndiye Yesu wa lile Jipya.” Mnakumbuka ile—ile—ile. . .

Nilipokuwa nikienda kuwinda kindi asubuhi ile, na hayo hapo, mashina hayo matatu yaliungana yakawa moja kule, moja kwa moja kule mlimani; huku mimi nimesimama pale nikiiangalia. Ndipo nikasogea karibu nikatoa kofia yangu, nikailaza chini bunduki yangu, nikapanda nikaenda kule. Na Sauti ikatikisa ule msitu, kasema, “Yesu Kristo wa Agano Jipya Ndiye Yehova wa la Kale. Endelea kuwa mwaminifu.” Kwa hiyo chini ya mahali pale ndipo wale kindi walitoka, wakati ule, wakaweko na huku hakukuweko na wowote pale. Mnaona? Hiyo ni Kweli. Mnaona? Ni kweli. Kwa hiyo, Mungu anajua, ambaye nasimama Mbele Zake, ni Ukweli wa jambo hilo. Hilo ni sawa. Ni Kweli.

123 Chini huko Kentucky; na kuna watu wameketi papa hapa usiku wa leo, waliokuweko jambo hilo lilipotukia tena, jambo lile lile. Naam. Tunajua hiyo ni Kweli; Yesu wa Agano la Kale!

¹²⁴ Kama wakati Wachina walipokuja huku mara ya kwanza, wao hawangeweza kusoma wala kuandika lugha yetu, bali walikuwa dobi hodari. Na kwa hiyo wao wange-... ungeshuka uende kwenye dobi ya Wachina. Alijichukulia tu kipande kidogo kisafi na cheupe cha kufungia. Yeye hangaliweza kusoma kitu, naye alijua hungaliweza kukisoma kama angalikiandika. Kwa hiyo, ulipokuja, yeye alichukua tu kipande hiki kidogo cheupe cha karatasi, kitu kama *hiki*, tuseme, papa hapa, naye akakirarua *hivi* kwa njia fulani. Sasa, alikupa kipande kimoja cha karatasi, akaweka hicho kipande kingine cha karatasi. Ndipo basi uliporudi kuchukua nguo zako, yeye alisema, “Hebu nikione kipande chako cha karatasi.” Naye akavichukua; kama vililingana, basi. Unazichukua nguo zako zilizokuwa chafu zikiwa safi.

¹²⁵ Naye Yesu alilingana na kila unabii; kila kiolezo cha Yehova wa Agano la Kale ni Yesu wa lile Jipya. Yeye alilingana na kila kitu.

Hebu niseme jambo hili kwa kicho cha kiungu na heshima, lakini upendo, lakini unyofu wa kujua ninakosimama. Ujumbe wa wakati huu umelingana na kila kitu kilichonenwa na Biblia kwa ajili ya saa hii. Sasa, iwapo una baadhi ya nguo chafu, zilete. A-ha. Umeoshwa kwa Damu ya Mwana-Kondoo?

¹²⁶ Angalia, “tukichukua shutumu Lake,” maana alikuwa Neno lililothibitishwa. Kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Waebrania 13:12 na 13. Tunaona Waebrania, 8, ama 13:8, pia. “Tukichukua aibu Yake,” ya Injili.

¹²⁷ Tukilichukua Jina Lake! Yeye alisema, “Nilikuja katika Jina la Baba Yangu.” Jina la Baba ni lipi? Yeye alikuja katika Jina la Baba Yake. Kasema, “Nilikuja katika Jina la Baba Yangu wala hamkunipokea.” Vema? Jina la Baba ni lipi? Nadhani yawapasa kujua. Mnaona?

Tukichukua shutumu la Neno. Daima lilichukuliwa nje ya kambi zao. Wakalitoa nje. Utachekwa, na kufanyiwa dhahaka.

¹²⁸ Na, leo, ambapo nilipoanza kwenda kila mahali nchini... Sikuzungumza habari zangu mwenyewe; tafadhali msifikiri hili ni jambo la kibinafsi. Lakini, wakati wangu umekwisha, nami nina yapata kurasa kumi hapa. Mnaweza kuona yaliyosalia hapa, mnaona, mnaona, vema, maandishi. Lakini, sikizeni. Kwanza ilianza...

¹²⁹ Mliona kwanza Yesu alipoanza? “Loo, yule Rabi kijana. Loo, Yeye alikuwa Mtu wa ajabu! Njoo kwetu. Njoo ukatuhubirie.”

¹³⁰ Lakini siku moja akawakemea, akasema, “Msipoula mwili Wake Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu.”

¹³¹ Mnadhani madaktari na wenye elimu wa hilo kundi waliwazia nini? “Mtu huyu ni kizuu kifyonza damu.” Mnaona? “Anawatakeni muinywe damu ya binadamu. Hilo limezidi mno kwetu. Mwacheni. Ma—makuhani walisema alikuwa na kichaa; naamini jambo hilo.” Nayo Biblia inasema waliondoka wakaenda zao.

¹³² Ndipo Yeye alikuwa na wahubiri sabini waliosimikwa. Naye akasema, “Siwezi kuwachukua.”

Kwa hiyo akageuka akawaangalia, akasema, “Mtasemaje mmwonapo Mwana wa Adamu akipaa huko Mbinguni alikokuwa kwanza?” Naam, Yeye hakuyaeleza mambo haya. Aliyaacha tu hivyo. Mnaona?

¹³³ Nao wakasema, “Mwana wa Adamu? Ati nini? Tunakula na Mtu huyu. Tunavua samaki pamoja Naye. Tunaketi ukingoni pamoja Naye. Tumeona kitanda kidogo alipopembezwa. Tunamjua mama Yake. Tunajua ndugu Yake. Ni nani anayeweza kupokea kitu kama Hiki?”

Nayo Biblia inasema, “Hawakuandamana Naye tena.”

¹³⁴ Kisha akamgeukia Petro na hao wengine, kasema, “Niliwachagua kumi na wawili, ninyi kumi na wawili.” Naam, kutoka yale maelfu, amepungukiwa akawa na kumi na wawili. Kisha akasema, “Niliwachagua kumi na wawili. Kisha, mmoja wenu ni ibilisi. Nilihua jambo hilo, tangu mwanzo.” Yeye akasema, “Sasa mnataka kwenda kuambatana nao?”

Haikumlazimu kuwabembeleza na kuwashawishi, na, “Nitakufanya shemasi kama utajiunga na kanisa.” Mnaona? Hamna mambo ya kisiri. Yeye hata hakulielezea. Wala hao wanafunzi hawakuweza kulielezea.

Lakini, mnakumbuka, Yeye aliwaambia tu, “Niliwajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Niliwachagua mkaipokee furaha pamoja Nami.” Mnaona? Ndivyo ilivyo, “kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,” walichaguliwa tangu zamani.

¹³⁵ Hao mitume walisimama pale imara vivyo hivyo. Hawangeeleza jinsi watakavyoula mwili Wake na kuinywa Damu Yake. Hakuweza kufahamu jinsi alivyopata kushuka, na huku amekuwa papo hapo pamoja nao wakati wote. Hakuweza kueleza jambo hilo. Hao watu wasingeweza kulieleza. Hakuna mtu angaliweza kulieleza.

Bali Petro alitamka maneno hayo makuu. Si ajabu alimpa yeye ufunguo. Akasema, “Bwana, tumwendee nani? Tumeshawishika. Tunajua ya kwamba Wewe, na Wewe pekee, Ndiwe thibitisho na Neno lililoahidiwa la siku hii. Tunajua ya kuwa Wewe pekee ndiwe uliye na Neno la Uzima. Sisi hatuwezi kuyaeleza mambo hayo, bali tunayaamini, hata hivyo.”

¹³⁶ Maskini Martha alisema, “Ndugu Yangu amekufa. Yeye yuko kaburini. Ameoza; ananuka. Bwana, kama ungalikuwapo

hapa, ndugu yangu hangalikufa. Lakini hata sasa, yo yote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupaa.” Loo, jamani!

¹³⁷ Yeye akasema, “Mimi Ndimi huo ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Naye kila aishiye na kuniamini, hatakufa kabisa hata milele. Je! unayasadiki haya?”

¹³⁸ Akasema, “Naam, Bwana. Siwezi kuyaeleza, bali nimeyasadiki. Nasadiki ya kwamba Wewe Ndiwe Kristo Yule ajaye ulimwenguni. Nasadiki, kwa Andiko linalojulikana sana, ya kwamba Wewe unalitimiza.”

¹³⁹ Kasema, “Mmemzika wapi?” Loo, jamani! Jambo fulani halina budi kutukia. Kila gurudumu linakuja pamoja wakati ufaao. Mnaona?

¹⁴⁰ Akashuka akaenda kaburini. Biblia ilisema, “Hakuwa na uzuri hata tumtamani.” Labda Jamaa mdogo aliyeinama mabega, alisimama huku mabega yameinama, amechoka na kudhoofika kwa kutembea.

Akasema, “Lazaro, njoo huku nje!” Na mtu aliyekuwa amekufa, siku nne, akasimama kwa miguu yake.

¹⁴¹ Mwanamke wa Christian Science. Samahani kama nikiwaudhi; sitaki kufanya hivyo. Mwanamke wa Christian Science, kutoka kanisa lili hili, alikutana nami huko nje siku moja. Naye akasema, “Bw. Branham,” akasema, “nayapenda mahubiri yako, bali kuna jambo moja umezidi sana kwayo!”

Nikasema, “Ni lipi hilo?”

Kasema, “Unajisifu sana juu ya Yesu.”

¹⁴² Nikasema, “Natumaini hilo tu ndilo Yeye alilo nalo dhidi yangu.” Mnaona? Mnaona? Mnaona?

¹⁴³ Akasema, “Unamfanya kuwa Mungu.” Mnaona, wao hawaamini alikuwa Mungu. Wao wanaamini alikuwa tu mtu wa kawaida, mwalimu bora, mfalsafa. Kasema, “Unamfanya kuwa Mungu. Naye hakuwa Mungu.”

¹⁴⁴ Nikasema, “Loo, naam, Yeye alikuwa hivyo.”

Akasema, “Kama nikikuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, Yeye si wa Kiungu, utaamini?”

¹⁴⁵ Nikasema, “Biblia yangu ilisema hivyo, na—naamini Neno. Hivyo ndivyo alivyo Yeye.”

Naye akasema, “Katika Yohana Mtakatifu, sura ya 11, wakati Yesu aliposhuka akaenda kwenye kaburi la Lazaro, Biblia ilisema alilia.”

Nikasema, “Hilo lina uhusiano gani nalo?”

Akasema, “Vema, hiyo inaonyesha ya kwamba hakuwa Mungu.”

¹⁴⁶ Nikasema, “Unakosa tu kuona huyo Mtu alikuwa ni Nani. Alikuwa wote wawili Mungu na mwanadamu. Na kama mwanadamu, akilia, alipokuwa analia kwa ajili ya huzuni yao. Bali aliposimama na kusema, ‘Lazaro, njoo huku nje,’ na mtu aliyekuwa amekufa, siku nne, akasimama kwa miguu yake tena, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu.” Naam, bwana! Naam, kweli!

¹⁴⁷ Nami mara nyingi nimetoa tamshi hili, aliposhuka kutoka mlimani usiku huo, ana njaa, Yeye alikuwa mwanadamu. Alisikia njaa kesho yake asubuhi. Yeye alikuwa mwanadamu. Bali alipochukua biskuti mbili na samaki watano, na kuwalisha elfu tano, wakaokota vikapu saba, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Naam, bwana. Yeye alikuwa mwanadamu, pale msalabani, alipolia, “Mungu Wangu, umeniacha?” Wakati alipolia, “Nipe maji ninywe,” nao wakampa siki na nyongo, Yeye alikuwa mwanadamu, akilia. Bali katika asubuhi ya Pasaka, wakati Yeye alipovunja kila muhuri wa mauti, kuzimu, na kaburi, kisha akafufuka, Yeye alikuwa zaidi ya mwanadamu.

¹⁴⁸ Yeye alikuwa mwanadamu usiku ule, amelala nyuma ya ile mashua alipokuwa kule pamoja na wanafunzi Wake, na pepo elfu kumi wa bahari wakaapa ya kwamba watamtosa majini. A-ha. Huko nje katika maskini meli ndogo ya kale, kama kizibo cha chupa kule nje, namna hiyo; alikuwa amechoka sana, hata hayakumwamsha. Yeye alikuwa mwanadamu alipokuwa amelala. Bali alipouweka mguu wake kwenye ubao wa ule mtumbwi, kisha akainua macho yake juu akasema, “Amani, tulia,” nao upepo na mawimbi vikamtii Yeye, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Ilikuwa Mungu!

Si ajabu yule mshairi alisema:

Maishani, alinipenda; kifoni, akaniokoa;
Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, akanihesabia haki bure milele;
Yuaa siku moja, Loo siku tukufu!

¹⁴⁹ Naam, bwana! Nenda nje ya kambi. Sijali inagharimu nini.

Msalaba huu uliowekwa wakfu nitaubeba
Hata kifo kitakaponiweka huru;
Kisha niende Nyumbani, nikavae taji,
Kwa maana kuna taji kwa ajili yangu.

¹⁵⁰ Nikifunga, nitasema hivi. Nilikuwa nikisoma hadithi moja juzijuzi, juu ya hakimu mmoja. Yeye alikuwa mtu wa haki, mtu mwema, alipendwa. Na kulikuwa na kundi la watu katika mji huo waliodhani ya kwamba wanaweza kuepuka cho chote, kwa hiyo, walikuwa na mali nyingi, kwa hiyo wakafungua nyumba yenye sifa mbaya, wakaendeleza duka la pombe, pombe, kila kitu namna hiyo. Ilikuwa haramu. Nao wakashikwa na sheria, mwanasheria wa taifa, nao wakapelekwa mahakamani. Na wakati watu wote wa mji, huo mji mdogo walipokusanyika,

walijua mtu huyu alikuwa amefanya mambo mengi sana hapo, mtu huyo aliyekuwa ameendeleza mahali hapo penye sifa mbaya. Nao—nao, lile baraza la mahakama, lilimpata mtu huyo na hatia, maana alishikwa katika kitendo. Na kwa hiyo huyo hakimku akampata na hatia, ndipo basi akapewa kifungo cha miaka kadha, bila dhamana, bila kukata rufani ama cho chote kile, alimfunga, kwa maana hivyo ndivyo sheria ilivyosema.

¹⁵¹ Watu waliokuwa nje ya mahakama wakashindana naye, wakasema, “Wajua nini? Kila mtu katika mji huu atakuchukia!” Kasema, “Wanakuchukia kwa kutoa uamuzi huo juu ya mtu yule.” Wote walikuwa wacheza kamari wao wenyewe. Ndipo wakasema, “So—sote tutakuchukia. Hatutakuchagua tena. Hakuna hata mmoja wetu atakayekupigia kura,” wakimzomea alipokuwa anashuka kwenda barabarani.

¹⁵² Naye akasimama kwa dakika moja, kasema, “Hebu niseme neno.” Akasema, “Nimeteteleza wajibu wangu kabisa. Huyu mtu alikuwa na hatia, hata awe ni nani. Nami ilinibidi kumhukumu kulingana na sheria ambayo niliapa nitaishindania.”

Akasema, “Unachukiwa katika mji huu!”

¹⁵³ Yeye akasema, “Lakini ninapendwa sana nyumbani, na watu wangu.”

¹⁵⁴ Huenda tukafikiria jambo lile lile, kama mtaniradhi kwa tamshi hilo. Nimetetea yale niliyookolewa kutekeleza, kushindania Neno hili la Mungu. Najua madhehebu yananichukia kwa ajili ya yale mambo ninayosema, bali mimi ninapendwa sana katika Nyumba Yake, miongoni mwa watu Wake.

Na tuombe.

¹⁵⁵ Bwana Yesu, huenda tukachukiwa na ulimwengu, bali tunapendwa na Baba. Tusaidie, Mungu Mpendwa. Wasaidie watu hawa, ili kwamba kila mmoja wao, Bwana, ya kwamba baraka Zako zitakaa juu yao. Hebu na twende nje ya kambi sasa. Hebu na twende nje ya mawazo yetu. Hebu na tuenende kulingana na mawazo ya Mungu. Nayu Biblia ilisema haya, “Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo ndani ya Kristo.” Kwa hiyo tujalie tuwazie mawazo Yake, si mawazo yetu, kwa maana karibu wakati wote sisi tumekosea. Kwa hiyo, tupate kuhakikisha, nia Yake na iwe juu yetu. Na nia Yake ilikuwa kutenda mapenzi ya Baba, na mapenzi ya Baba ni Neno Lake lililoahidiwa.

¹⁵⁶ Tujalie twende nje ya kambi, usiku huu, Bwana, tukampate Yesu. Hatutampata kamwe kwa kujiunga na kanisa. Hatutampata kwa kupeana mikono na hudumu fulani, ama—ama kutia sahihi kanuni fulani za imani, ama kitu fulani tulichoahidi, kuhudhuria shule ya Jumapili kwa siku kadha

katika mwaka, na kadhalika. Tutampata tu katika Neno, kwa maana Yeye ni Neno.

¹⁵⁷ Na tunapona siku hii iliyoahidiwa, ya kwamba atakuwa nje ya kambi, ametolewa nje tena; sasa hebu twendeni nje ya kambi, tukiwa tayari kuchukua shutumu Lake; tumechukiwa na ulimwengu huu, bali tumependwa na Yeye Yule ambaye ametualika katika Kambi. Tujalie, Bwana.

¹⁵⁸ Iwapo hapa kuna wale wasiomjua Yeye, nao hawajaenda nje ya kambi kamwe ya ushirika wa kanisa fulani, na hata hivyo unakiri kuwa Mkristo. Lakini unaposema, “Mambo haya, naamini, ni kwa ajili ya siku nyingine,” hiyo inaonyesha haiwezi kuwa ni Roho Mtakatifu.

Mtu aliyejazwa na Roho mtakatifu anawezaje kubatizwa akitumia jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu”? Wakati, Paulo, yule mtume maarufu, alisema, “Kama Malaika akishuka kutoka Mbinguni...” Huenda ulitenda jambo hilo, wakati mmoja, bila kujua tofauti yake. Hao watu walifanya jambo hilo, bila kujua jambo tofauti, katika Matendo 19. Bali yeye alisema, “Malaika akihubiri jambo lingine lo lote, na alaaniwe.”

Unawezaje kukubali kanuni fulani za imani, ama itikadi fulani, kitu kingine kile, wakati Biblia ilisema, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu,” jambo lili hili, “ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu”?

¹⁵⁹ Roho Mtakatifu anawezaje, Yeye aliyeliandika Neno, kuwa ndani yako, akilikana Neno? Anawezaje kulikana, wakati Roho Mtakatifu yule yule Mwenyewe alisema, “Kama mtu ye yote ataongeza neno moja kwa Hili, ama aondoe cho chote toka Kwalo, nitaitoa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima”? Roho Mtakatifu basi anawezaje kutoa cho chote kutoka kwenye Neno, ama kuongeza lo lote kwenye Neno?

¹⁶⁰ Rafiki yangu, hapa na katika ulimwengu usioonekana kwa macho ambako kanda hii itakwenda, ambao hatuwaoni sasa, hebu hayo yaingie kwenye kilindi cha moyo wako kutoka kwenye Ujumbe wa mafundisho ya asubuhi ya leo, kuona mahali tulipo sisi. Kama hujapokea maagizo haya bado ambayo nimezungumzia muda mfupi uliopita, mbona usiyapokee? Tuko hapa kufanya kila tuwezacho kwa ajili yako, kukusaidia.

¹⁶¹ Mimi ni shahidi tu. Mimi ni mpiga kampeni tu. Kama tulivyo nao huko Luoisville sasa, M—Mkutano mkubwa wa Democrat wa Kentucky, ule... Wao wanamjengea jukwaa mtu wao atakayechaguliwa. Nami pia najenga jukwaa kwa ajili ya Bwana wangu. Mbona usimpokee, usiku wa leo, kama wako?

¹⁶² Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu, pia, katika wakati huu, waweza tu kuinua mikono yako na kumwambia Mungu. Si kwa ajili yangu mimi; mimi ni mwanadamu tu. Mwinulie Mungu mikono yako, useme, “Mungu, nirehemu. Kweli nataka mambo haya ambayo nimesikia habari zake. Nataka kwenda nje ya kambi. Sijali asemayo mtu ye yote.”

Mungu awabariki. Jamani, hiyo mikono, hiyo mikono! “Nataka kwenda nje ya kambi. Haidhuru itanigharimu nini, nitautwaa msalaba wangu na kuubeba kila siku. Nitatoka nje ya kambi. Hata watu waseme nini juu yangu, nataka kumfuata nje ya kambi. Niko tayari kwenda.”

¹⁶³ Baba wa Mbinguni, umeiona mikono hiyo. Labda watu mia moja, ama zaidi, jengoni, waliinua mikono yao. Bwana, kuna Kitu fulani karibu nao sasa, Mtu mwingine, Utu wa Kristo, usioonekana kwa macho ya kawaida, nao umewafanya kufanya uamuzi. Katika maisha yao wenyewe, wanajua wanapoangalia kwenye kioo, wanaona kwamba kuna kitu fulani ambacho hakipo. Nao wanataka maisha yao yapangwe kulingana na ahadi ya Mungu, nao wameinua mikono yao kwa unyenyekevu mkuu. Wasaidie, Bwana, waelekee kwenye ule mlango mkubwa usiku wa leo, kwenye zizi la kondoo. Jalia waingie vizuri na kwa unyenyekevu. Tujalie. Hao ni Wako, Bwana. Washughulikie.

¹⁶⁴ Sasa, hawangaliweza kufanya uamuzi huo, hawangaliweza kuinua mikono yao, bila kitu fulani cha kimbinguni. Inaonyesha kuna uzima hapo mahali fulani. Kwa kuwa, kulingana na sayansi, nguvu za uvutano zingeishikilia mikono yetu chini. Bali kuna kitu kilichogusa nia yao, ambacho kiliwafanya kuasi sheria ya nguvu za uvutano na wakainua mikono yao wakiielekeza kwa Muumba aliyewaleta. “Naam, nataka kwenda umbali wote. Nataka kwenda nje ya kambi, usiku wa leo.”

¹⁶⁵ Bwana, kidimbwi ki tayari kwa ajili ya hatua ya kwanza baada ya kutubu, kisha kubatizwa, na ahadi ya kumpokea Roho Mtakatifu. Katika siku hizi za mwisho, kuitwa kuirudia ile Imani ya asili, maagizo yale ya awali! Tunawaona watu wengi sana walio mbali na Kristo, wakifa kwa maagizo haya mengine yaliyoandikwa na wanadamu. Huenda wakawa ni wazuri sana katika madhehebu yao, lakini, Bwana, na—nataka maagizo Yako.

Wewe Ndiwe Daktari wetu. Kuna Daktari. Kuna zeri Gileadi. Kuna Tabibu hapa, usiku wa leo, kuiponya kila nafsi iliyolemewa na dhambi, kumponya kila mtu mwenye mwili. Ewe Daktari mkuu wa nyakati zote, ewe Muumba mkuu wa mbingu na nchi, njoo sasa, tafadhali, miongoni mwetu, na uzungumze nasi. Katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁶⁶ Huku kila mmoja akiomba moyoni mwake, “Bwana Yesu, nisaidie sasa!” Na kama hujawahi kubatizwa, nawe umeshawishika... Sijahubiri juu ya ubatizo. Bali umeshawishika ya kwamba huna budi kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo, njia tu ambayo Mkristo ye yote... .

¹⁶⁷ Vipi kama ungelikuja Kule, huku umebatizwa kwa njia nyingine, na Yesu yeye yule aliyesema, “Ye yote atakayeliondoa Neno moja, ama aongeze Neno moja, huyu sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima”? Yesu alisema hivyo.

Kisha akasema, “Maandiko yote yana pumzi na hayana budi kutimizwa.” Sasa unajua vinginevyo. Utafanyaje juu ya jambo hilo?

¹⁶⁸ Kama umekuwa tu na msisimko ama cho chote kile! Mimi naamini katika msisimko. Kama tu umecheza katika Roho, ukanena kwa lugha! Naamini katika jambo hilo, pia. Bali kama ulienda umbali huo pekee, na roho iliyo ndani yako inakuambia usilifuute Neno wakati unajua ya kwamba ni kweli, roho huyo ana kasoro. Si Roho Mtakatifu. Haiwezi kuwa. Mnaona, angetambua Neno Lake Mwenyewe. Unajua hivyo. Unaweza kujitayarisha kuja wakati tunapoomba.

¹⁶⁹ Yesu wa Nazareti, njoo karibu sasa ukazungumze na kila moyo. Nawakabidhi Kwako. Na wawe, mikono hii yote, wote ni kumbukumbu vya Ujumbe, Bwana, kutoka Kwako, Uwepo Wako mkuu wenye utukufu ulio nasi sasa. Mtu ye yote mwepesi wa kuhisi Roho anaweza kujua Wewe uko hapa, huku kuhisi kukuu kwa utakatifu. Tujalie, Bwana, sasa hivi, katika Jina la Yesu Kristo.

Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

¹⁷⁰ Iwapo kuna mtu hapa ambaye angetaka kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, anataka kutubu, anataka kutafuta ubatizo wa Roho, kuna chumba kilicho wazi mkono wangu wa kushoto; wanawake, upande wa kulia. Kutakuweko na mtu huko wa kukupa maelezo. Kuna majoho ya ubatizo yanayongoja, kila kitu.

¹⁷¹ Sasa, huku tumeviinamisha vichwa vyetu, tukiimba, “Naweza kumsikia . . .” Tutakutana nanyi.



KUENDA NJE YA KAMBI SWA64-0719E

(Going Beyond The Camp)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jinni, tarehe 19 Julai, 1964 katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org